TANGAZO LA SERIKALI NA. 276 la tarehe 12/4/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA YA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA SHUGHULI ZA UVUVI ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA ZA MWAKA 2024

Jina na Matumizi

**1**. Sheria ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Shughuli za Uvuvi za Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga za mwaka 2024 na zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

Tafsiri

**2**. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa Uvuvi aliye au asiye na taaluma ya Uvuvi au Afisa au Mtumishi yeyote anayeruhusiwa au kuteuliwa na Mkurugenzi kwa maandishi kutekeleza wajibu wowote kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Afisa Uvuvi" maana yake ni Mtumishi wa Serikali aliye chini ya Utumishi wa Halmashauri katika Sekta au Idara ya Uvuvi kuanzia cheo cha Afisa Uvuvi Msaidizi Daraja la IV;

"baruti" maana yake ni bomu au mlipuko wa bomu ambao unasababisha uharibifu wa mazingira na kuuwa viumbe, samaki na mazalia yao katika sehemu mlipuko huo ulikofanyika;

"chombo cha uchukuzi" maana yake ni chombo cha usafiri wa majini au nchi kavu kilichotengenezwa maalum kwa ajili ya kutumika kubeba, kusafirisha au kuchukua samaki wakavu au wabichi kwa kutumia vibebea barafu na chombo hiki kinaweza kuwa gari, boti, karua, ngama, mashua ya kutumia injini, mashua, mtumbwi wa kutumia joshi au kasia;

Sura ya 279

"chombo cha uvuvi" maana yake ni chombo kilichoandikishwa au ambacho hakijaandikishwa na

kilichokatiwa au ambacho hakijakatiwa leseni ya uvuvi chini ya Sheria ya Uvuvi;

"dandali" maana yake ni vipande viwili vya fito vilivyotengenezwa kwa duara au namna nyingine yoyote na kusukwa kwa kamba na miti,katani au manila na hutumika kufungia samaki wakavu wakati wa kusafirisha kwenda kuwauza;

"eneo la kuanika Samaki" maana yake ni eneo la ardhi lililotengwa na Serikali au jamii lililopo katika ufukwe wa ziwa (Mwaloni) lenye urefu wa mita zipatazo sitini kutoka ufukweni hadi nchi kavu lenye mchanga au nyasi fupi fupi linalotumiwa na wavuvi kuanika samaki;

"gunia" maana yake ni mfuko mkubwa uliotengenezwa kwa kamba za katani, nailoni, politheni au viloba kwa madhumuni ya kuchukulia samaki au dagaa na kutumika kufungia samaki wakavu au wabichi wakati wa kuwasafirisha;

"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga;

"Kampuni" maana yake ni kampuni au kiwanda cha samaki kilichosajiliwa kisheria kinachojishughulisha na ununuzi au ukusanyaji wa samaki kwa kutumia wafanyakazi wake au mawakala kwa madhumuni ya kutengeneza au kusindika samaki kiwandani;

"kutengeneza samaki" maana yake ni kukata katika vipande vipande visivyo au vyenye mifupa, kuweka barafu, kufukiza, kuhifadhi au kukausha kwa kutumia chumvi (Kayabo), kukaanga au kuhifadhi samaki kwa njia au namna yoyote ile kwa madhumuni ya biashara;

"kuuza nje" maana yake ni kutoa bidhaa zitokanazo na uvuvi na mazao yake katika Halmashauri ya Mwanga na kupeleka mahali popote nje ya eneo la Mamlaka ya Halmashauri;

Sura ya 279

"mchuuzi wa samaki" maana yake ni Mtu binafsi, kikundi cha watu, Taasisi, Kampuni, Shirika au Chama kinachojihusisha au kushughulika na biashara ya samaki au bidhaa yoyote ya Samaki kwa kununua, kuuza kutengeneza au kusafirisha samaki hao au mazao yake kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa

Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga au Mtu aliyeteuliwa kukaimu nafasi hiyo na kutekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Mvuvi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, Taasisi au Shirika linalojishughulisha na shughuli za uvuvi katika Wilaya ya Mwanga;

"Mwalo" maana yake ni eneo lililopo kando kando ya ziwa, bwawa au sehemu yoyote ile inayotumiwa na wavuvi kutua, kupakua au kupakia samaki, zana za uvuvi na bidhaa nyinginezo kwa madhumuni ya biashara au matumizi ya nyumbani;

"sumu" maana yake ni dawa zinazotokana na miti aina ya mruku au mti wowote ule ambao majani yake, magome au mizizi ya miti hiyo iliyopondwa pondwa na kutengenezwa madawa ya kienyeji au dawa inayotokana na kemikali za viwanda ambayo hutumika kuwalewesha au kuwaua samaki na zina madhara kwa binadamu;

"Tenga" maana yake ni chombo ambacho kimetengenezwa kwa mianzi au matete ambacho kinatumika kusafirisha bidhaa za mazao ya uvuvi na Tenga nne ni sawa na dandali moja kwa maana ya tafsiri ya utozaji ushuru wa Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu, Taasisi, Kampuni au mtu aliyepewa uwakala wa kukusanya ushuru wa samaki na Halmashauri na inahusisha Watumishi wa Wakala huyo waliopewa vitambulisho vilivyosainiwa na Mkurugenzi vyenye kuonyesha aina ya uwakala na mwaka walioruhusiwa kukusanya ushuru huo; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mita.

Utaratibu wa Ada ya Leseni na ushuru wa mazao yanayotokana na uvuvi

**3**.-(1) Halmashauri itatoza Ada ya Leseni kwa vyombo vya uvuvi na ushuru kwa mazao yanayotokana na uvuvi kama ilivyoainishwa katika Jedwali

(2) Mtu au taasisi inayofanya biashara ya samaki au kujishughulisha na shughuli za uvuvi itatakiwa kuwa na leseni kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

Wajibu katika Sheria Ndogo

**4**.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila Kampuni, Mtu au Watu wanaojishughulisha na kukusanya au kununua samaki

hizi

au mazao yake kwa kutumia, gari, mtumbwi, karua, ngama au chombo kingine chochote cha kusafirisha samaki na mazao yake ndani ya eneo la Halmashauri kuhakikisha kwamba inaomba na kupata kibali cha Halmashauri.

(2) Mtu binafsi endapo atakusanya Samaki kwenye Halmashauri kwa kutumia mashua, mtumbwi, karua, ngama, gari au sanduku la kuhifadhia samaki atatakiwa kutuma maombi kwa Mkurugenzi akionesha aina ya chombo atakachotumia kukusanyia na kusafirishia Samaki.

(3) Maombi yaliyotumwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (2) yakipokelewa na kukubaliwa, mtu huyo atapaswa kusaini mkataba wa kulipa ushuru wa samaki kwa Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

(4) Kampuni, Mtu au Taasisi ambayo imekubaliwa maombi yake itapewa fomu na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

(5) Ushuru wa Samaki utakusanywa na Afisa Uvuvi, Afisa Mwidhiniwa, Mkusanya Ushuru au Wakala wa Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(6) Mmiliki wa chombo cha Uvuvi, Mtumishi au Msimamizi wake aliyemteua atapaswa kutoa ushirikiano kwa Afisa Uvuvi, Afisa Mwidhiniwa, Mkusanya Ushuru au Wakala wa Halmashauri kuhakikisha kuwa ushuru wa samaki unalipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(7) Ushuru wa samaki na mazao yake hautatozwa mara mbili kwa samaki au bidhaa iliyokwisha kulipiwa ushuru wa Halmashauri katika sehemu nyingine ndani ya Halmashauri;

(8) isipokuwa muhusika atapaswa kuonyesha stakabadhi ya ushuru aliyolipia kutoka sehemu aliyolipia samaki au bidhaa yake ndani ya eneo la Halmashauri kwa ajili ya uhakiki au ukaguzi.

Kipindi cha kulipa leseni za uvuvi

**5**.-(1) Kutakuwa na kipindi cha kulipa Ada ya Leseni ya vyombo vya uvuvi, wavuvi na wafanyabiashara wa samaki ambacho kitakuwa ni kuanzia Januari moja mpaka machi thelathini na moja ya kila mwaka.

(2) Mara baada ya kipindi hicho kupita mmiliki wa chombo atapaswa kulipia Ada inayotakiwa pamoja na faini kwa mujibu wa sheria ndogo za ada na ushuru za Halmashauri.

(3) Mtu hataruhusiwa kufanya biashara ya

kuuza,kuvua au shughuli yoyote ya uvuvi bila ya kuwa na leseni ya uvuvi iliyo hai.

Makosa

**6**. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi itakuwa ni kosa kwa-

(a) Mtu kutoka nje ya eneo la Halmashauri kufanya shughuli za uvuvi bila kuripoti Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na kupata kibali kilichoainishwa katika Jedwali;

(b) Mmiliki, Msimamizi au mwenye chombo cha uchukuzi kupakia au kusafirisha mzigo wowote wa samaki, au bidhaa nyingine zinazotokana na samaki kutoka katika mwalo au eneo la Halmashauri kabla ya kulipiwa ushuru wa Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika sheria ndogo hizi, sheria ndogo ya ada na ushuru ya Halmashauri au sheria nyingine za nchi;

(c) Kampuni, taasisi, Mtu au kikundi cha watu kuvua samaki kwa kutumia nyavu za makila chini ya ukubwa wa macho ya inchi tatu au nyavu zozote zile zilizokatazwa kisheria;

(d) kuvua au kuua samaki wadogo ambao hawajakua kufikia kiwango cha kuvuliwa;

(e) kufanya shughuli za uvuvi na kusafirisha samaki nyakati za usiku bila ya kulipa ushuru;

(f) kumzuia, kumgomea au kumshambulia Afisa Uvuvi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala wakati anapotekeleza mojawapo ya majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(g) kufanya biashara ya uvuvi au kuuza samaki au mazao yatokanayo na Samaki bila Leseni; na

(h) kusafirisha samaki wabichi ambao hawajapimwa.

Maeneo maalum ya mazalio ya samaki

**7**.-(1) Kutakuwa na maeneo yaliyotengwa maalum kwa ajili ya mazalio ya samaki ambayo shughuli zozote za uvuvi hazitaruhusiwa wakati wote wa kipindi cha samaki kuzaliana na maeneo hayo yatatangazwa na Afisa Uvuvi.

(2) Mtu hataruhusiwa kuvua samaki katika maeneo yatakayoainishwa na Afisa Uvuvi kuwa maeneo ya mazalio ya samaki.

(3) Mtu hataruhusiwa kuvua samaki kwenye eneo au

ukanda wa mazalio ya samaki wakati msimu wa mazalio ya Samaki utakapokuwa umefungwa.

(4) Mtu hataruhusiwa kuingia au kupita kwenye sehemu au eneo la ukanda au mazalio ya samaki wakati ukanda huo umefungwa kwa shughuli za mazalio ya samaki isipokuwa kama kutakuwa na hali ya hewa mbaya kama vile tufani ambayo italazimisha chombo kwenda mrama hadi kuingia, kupita au kuelekea ukanda huo na mwenye chombo awe amefanya jitihada zote na jitihada hizo zimeshindikana.

Vituo, mwalo na maeneo maalum ya kuuza, kupokea na kusafirisha samaki

**8**.-(1) Kutakuwa na vituo, mialo au maeneo ya kupokelea, kuuza na kusafirisha samaki ambayo yatatumika kama sehemu maalum zilizoidhinishwa kwa shughuli za kununua na kusafirisha Samaki na maeneo hayo ni kama yalivyoainishwa katika Jedwali.

(2) Mtu hataruhusiwi kuuza, kununua au kusafirisha samaki nje ya maeneo, vituo na mialo iliyoruhusiwa au kutengwa kama vituo, mialo na sehemu za kuuzia, kununua na kusafirisha samaki isipokuwa sokoni na kwenye mialo au maeneo ya vivuko kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

(3) Mtu, Taasisi, Mamlaka, Kampuni, Mfanyabiashara au mvuvi atakayepuuza au kukataa kununua au kusafirisha samaki kwa kutumia sehemu zisizoruhusiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa.

Kushindwa kulipa ada na ushuru

**9**.-(1) Mtu, kikundi cha watu, Taasisi, Mamlaka, Kampuni, mfanyabiashara au mvuvi atakayeshindwa kulipa au kukwamisha au kusababisha kutolipwa kwa ushuru wa Samaki anatenda kosa.

(2) Mazao ya samaki ambayo hayajalipiwa ushuru, hayataruhusiwa kusafirishwa kutoka eneo la Halmashauri bila kuwa yamelipiwa ushuru na kuwa na kibali.

Sura ya 290

(3) Endapo kutatokea ukaidi wa kulipa ada au ushuru, mhusika atatakiwa kulipa ushuru anaodaiwa pamoja na kulipishwa faini kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa.

Usajili wa vyombo vya uvuvi

**10**.-(1) Vyombo vya Uvuvi vinatakiwa kusajiliwa na Halmashauri na endapo chombo hakitasajiliwa, mmiliki wa chombo husika atatakiwa kukisajili na kulipa faini ya asilimia hamsini ya ushuru ili kufidia gharama za ufuatiliaji na endapo muhusika atashindwa kulipia chombo chake

ndani ya saa ishirini na nne, Halmashauri au Wakala atataifisha chombo husika na kukiuza kwa mnada kufidia gharama pamoja na ushuru.

(2) Chombo cha uvuvi au usafiri wa majini hakitatakiwa kujirudia namba ya usajili na itakapobainika kuwa chombo au vyombo vya uvuvi au usafiri wa majini kimejirudia namba ya usajili Halmashauri itataifisha vyombo vyote ambavyo vimejirudia namba na itaviuza kwa mnada.

Adhabu

**11**. Mtu ambaye atakuwa ametenda kosa au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi ambacho adhabu yake haikutajwa atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi Milioni moja au kifungo kisichopungua miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(1),(2), 4(2),(3),(4),6(a),8(1),(2))*

**SEHEMU YA KWANZA**
**ADA YA LESENI**

| **Namba** | **Aina Ya Leseni** | **Ada Ya Leseni Kwa Mwaka (Tshs)** |
|---|---|---|
| 1. | Leseni ya Biashara ya Samaki | 23,000/= |
| 2 | Leseni ya Uvuvi | 23,000/= |
| 3 | Leseni ya chombo cha uvuvi | 23,000/= |

**SEHEMU YA PILI**
**KIPIMO NA KIWANGO CHA USHURU**

| **Namba** | **Kipimo** | **Aina Samaki** | **Kiwango Cha Ushuru** |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndoo ya Lita 20 (Wakavu/wabichi) | Perege, Kambale | 2,000@ndoo |

**SEHEMU YA TATU**

**KIBALI CHA KUENDESHA SHUGHULI ZA UVUVI**

**Picha ya Muombaji**

**KIBALI CHA KUENDESHA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA**

Namba ya Leseni……………………Namba ya Simu……………………….

Kibali kinatolewa kwa Bwana/Bibi/Bi./Ndugu………………………………

Ambaye ni mkazi wa……..……………Wilaya ya……………………………

Mkoa wa ………………………………………………. kufanya shughuli za uvuvi/ununuzi/ usafirishaji wa Samaki kutoka eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

Kibali hiki kitatumika kuanzia tarehe ………. mwezi wa ……Mwaka…………

Mpaka tarehe ………………. mwezi……………………………… mwaka……………

Mwombaji wa kibali amelipa malipo yote yanayohusiana na kibali hiki kwa stakabadhi

Na……………………………….ya tarehe …….. mwezi…………….. mwaka……….

……………………………………………..
**Afisa Uvuvi**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA**
**SEHEMU YA NNE**

**SEHEMU YA MAENEO YA VITUO, MIALO, SOKO LA SAMAKI AU SEHEMU YA KUEGESHA MITUMBWI AU KUUZIA, KUNUNUA NA KUSAFIRISHA SAMAKI WILAYA YA MWANGA**

| Namba | Tarafa | Kata | Kijiji | Kituo/Mwalo/Soko la Samaki |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Lembeni | Kirya | Nijapanda | National |
| | | | Kiti cha Mungu | Kiti cha Mungu |
| 2. | Mwanga | Lang'ata | Lang'ata Bora | Lang'ata Bora |
| | | | Kagongo | Kagongo |
| | | | Nyabinda | Nyabinda |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | Handeni | Bunge |
| 3. | Jipendea | Jipe | Jipe | Jipe |
| | | | Kambi ya simba | Ubembe |
| | | | Butu Ugweno | Mkisha |
| | | Kigonigoni | Ruru | Ruru |